MAELEZO YA MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, KATIKA HAFLA YA MKUTANO WA KWANZA WA KITAIFA WA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050 UKUMBI WA MIKUTANO WA JAKAYA KIKWETE, DODOMA

Jumamosi Tarehe 09 Disemba 2023

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar

Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar

Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mheshimiwa Dkt. Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri mliopo;

Mheshimiwa Rosemary Sitaki Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;

Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti n Waheshimiwa Wabunge wengine mliopo;

Mheshimiwa Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi;

Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu mliopo;

Waheshimiwa Mabalozi, Washirika na Wadau wa Maendeleo;

Viongozi wa Mashirika ya Dini;

Ndugu Wanahabari;

Mabibi na Mabwana.

“Jamhuri ya Muungano wa Tanzania”

1. ***Mheshimiwa Rais***, kwa niaba ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), ninayo heshima kubwa kukushukuru sana kwa kukubali kushiriki nasi katika tukio hili, na hususan kukubali kuwa Mgeni Rasmi. Uwepo wako hapa umetutia moyo sana na kuupa mchakato wa kuandika Dira ya Taifa ya Maendeleo msukumo na nguvu mpya.
2. ***Mheshimiwa Rais,*** ninaomba kutumia nafasi hii kuendelea kukupa pole wewe binafsi na watanzania wote kwa janga lililoikumba Wilaya ya Hanang na hususan wananchi wa Katesh. Tunakushukuru kwa moyo wako wa faraja. Tunawaombea wote waliofariki katika janga hili Mungu awape pumziko la amani. Aidha, tunawaombea majeruhi wote wapone haraka na kuendelea na shughuli zao za kila siku.
3. ***Mheshimiwa Rais,*** ninaomba pia niwashukuru wote walioitikia mwaliko wetu na kuweza kuhudhuria hafla hii. Kwa kipekee tunawashukuru mabalozi na wawakilishi wa taasisi za kimataifa na wote waliotoka nje ya Dodoma kwa kuweza kujumuika nasi.
4. ***Mheshimiwa Rais***, katika maelezo yangu ninaomba kuleta kwako mambo mawili. Jambo la kwanza ni muhtasari wa taarifa ya kitafiti ya tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, awamu ya kwanza. Awamu ya pili ya tathmini itafanyika baada ya muda wa Dira ya sasa kukamilika. Jambo la pili nitawasilisha kwako Timu Kuu ya Kitaalam itakayoratibu mchakato wa kuandika Dira.
5. ***Mheshimiwa Rais***, katika kipindi cha miaka 23 iliyopita, tangu mwaka 2000, mipango ya maendeleo ya nchi yetu inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Dira hii ina maeneo makubwa matano yafuatayo: **hali ya juu ya maisha bora; amani, utulivu na umoja**; ***utawala bora***; ***jamii iliyoelimika na yenye ari ya kujifunza***; na ***uchumi imara, endelevu na wenye faida kwa wote***. Kwa kuzingatia maeneo haya, ninaomba nieleze mafanikio katika maeneo tisa kwa muktadha wa mkutano huu. Ripoti kamili ya tathmini itakuwa wazi kwa umma na kila mtu ana uhuru wa kuchambua taarifa zilizopo katika ripoti hii.

Jedwali: **Muhtasari wa Mafanikio ya Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025**

Eneo lililopimwa	***Hali ilivyokuwa 2000***	***Hali ilivyo ilivyo 2022***	***Lengo 2025***
I: KULINDA AMANI, UTULIVU NA MSHIKAMANO WA KITAIFA			
II: KUJITOSHELEZA KWA CHAKULA NA LISHE			
1. Kujitosheleza kwa chakula	90%	124%	130%
2. Kupunguza kiwango cha watoto wenye udumavu	48%	30%	20%
3. Kupungua kwa kiwango cha watoto wa umri wa chini ya miaka mitano wenye uzito wa chini (underweight)	25.3%	2%	0%
III: ELIMU			
4. Kuongeza kiwango cha uandikishwaji cha watoto katika elimu ya msingi	69%	108.5%	100%
5. Kuongeza kiwango cha uandikishwaji cha watoto katika elimu ya sekondari	Chini ya 20%	48.2%	48%
6. Kuongeza kiwango cha watoto wanaohitimu elimu ya msingi	51%	69%	80%
7. Kuongeza kiwango cha wanafunzi wanaoendelea na elimu ya sekondari (kutoka drs VII kwenda kidato cha I)	20%	70%	90%
IV: AFYA			
8. Kupunguza idadi ya vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kwa kila akina mama 100,000	760	104	265
9. Kupunguza idadi ya vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano katika kila watoto 1000 wanaozaliwa	95	43	36
V: MAJI			
10. Upatikanaji wa maji vijijini	32	77	85
VI: UMEME			
11. Upatikanaji wa umeme	10%	78%	90%
VII: MIUNDOMBINU			
12. Kuongeza mtandao wa barabara za mikoani (KM ya barabara za lami na zege)	4,179	11,966	13,000
13. Umilikaji wa simu za mkononi (Kaya zenyeangalau simu moja ya mkononi)	30%	86%	100%
14. Watumiaji wa Internet (milioni)	13.2 (2010)	34.5	-
15. Watumiaji wa mitando ya kijamii (social media-	-	16.7	-

Eneo lililopimwa	*Hali ilivyokuwa 2000*	*Hali ilivyo ilivyo 2022*	*Lengo 2025*
milioni)			
VIII: KUONGEZA UMRI WA KUISHI	***52***	***66***	***68***
IX: KIPIMO CHA MAENDELEO YA WATU (HUMAN DEVELOPMENT INDEX-HDI)	***0.40***	***0.55***	***0.65***
X: ***KUJENGA UCHUMI IMARA NA SHINDANI KATIKA MSINGI WA VIWANDA*** *(semi-industrialised economy)* 16. Wastani wa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha miaka 20 ni 6.1% 17. Katika kipindi chote cha miaka 22 mfumuko wa bei ulibaki kuwa tarakimu moja, isipokuwa mwaka 2008 (10.3%) na mwaka 2009 (12.1%) 18. Mchango wa sekta za viwanda, ujenzi na uzalishaji katika pato la taifa uliongezeka kutoka 24.3% mwaka 2000 hadi 35.6% mwaka 2022 19. Mauzo nje ya nchi kutokana na bidhaa za viwandani yaliongezeka kutoka ***43.1 milioni*** (dola za kimarekani) mwaka 2000 hadi ***1,321.6 milioni*** (dola za kimarekani) mwaka 2022 20. Kwa ujumla, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka kutoka dola za kimarekani ***milioni 975*** mwaka 2000 hadi dola za kimarekani ***bilioni 5.91*** mwaka 2020.			

6. ***Mheshimiwa Rais,*** kwa wastani, watafiti waliofanya tathmini hii, Taasisi ya Tafiti za Kiuchumi na Kijamii – ESRF, wanakadiria kuwa hadi mwaka 2022 malengo yaliyowekwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 yamefikiwa kwa kiwango cha asilimia 60. Kwa ujumla wake, viashiria vya mafanikio katika sekta za huduma za jamii yanaonekana kuwa makubwa kuliko viashiria vya mafanikio katika sekta za kiuchumi. Hali hii inaweza kuwa inachangiwa, pamoja na mambo mengine, na kuendelea kukua kwa sekta isiyo rasmi na hivyo baadhi ya takwimu za kiuchumi kutokupatikana kirahisi.
7. ***Mheshimiwa Rais,*** pamoja na mafanikio tuliyoyapata, mambo mawili yafuatayo ni dhahiri:
    i) Katika kipindi cha utekelezaji wa Dira ya sasa, mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi yaliendelea kutawaliwa na usafirishaji wa mali ghafi bila kuongezea thamani.
    ii) mchango wa sekta ya ***kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda*** bado ni mdogo katika pato la taifa. Ni kwa sababu hii, kasi ya ukuaji wa uchumi imekuwa haiendani na

kasi ya kupunguza umaskini na kuzalisha ajira, hususani katika maeneo ya vijijini ambako wananchi wengi wanajishughulisha na sekta hizi.

8. ***Mheshimiwa Rais***, ni katika muktadha niliioeleza hapo juu, Serikali yako imeweka msukumo wa kipekee katika sekta ya kilimo kama inavyodhihirika katika kuongezeka kwa bajeti ya kilimo. Aidha, Serikali yako imeweka mkazo mkubwa katika kuvutia na kuchochea uwekezaji katika sekta ya viwanda na uzalishaji na kukuza biashara. Maono yako haya na msukumo wako huu katika maeneo haya itakuwa ni msingi muhimu kwa Dira ijayo.
9. ***Mheshimiwa Rais***, pamoja na mambo mengine, Dira ijayo itaweka mkazo katika ***kuchochea kasi ya ukuaji uchumi ambao ni jumuishi, unaopunguza umaskini, unaozalisha ajira kwa wingi, na unaochochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi***, kwa lengo la ***kukuza ustawi kwa wote*** (***prosperity for all***). Hatua hizi ni pamoja na kuweka msukumo katika kuongeza tija ya uzalishaji na uongezaji thamani katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini; kuchochea na kuboresha ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote; kuongeza na kuimarisha matumizi zaidi ya teknolojia, hususan teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika zama hizi za mapinduzi ya nne ya viwanda; kuongeza uzalishaji viwandani; na kuimarisha huduma bora za jamii kwa wote.
10. ***Mheshimiwa Rais,*** baada ya maelezo haya, sasa ninaomba kuwasilisha kwako wajumbe wa Timu Kuu ya Kitaalam itakayoratibu mchakato wa Dira ijayo kwa kushirikiana na Sekretariati ya Tume ya Mipango na kwa usimamizi wa karibu wa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Dira chini ya uenyekiti wa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Jedwali 2: **Majina na Wasifu wa Wajumbe wa Timu Kuu ya Kitaalam ya Dira (wajumbe 22)**

Jina na Taarifa za Mjumbe	***Muhtsari wa Wasifu wa Mjumbe***
1. Prof. Lucian Ambrose Msambachika (Kiongozi wa Timu) *Anwani: S.L.P 35045 DSM* *Email: msambi2000@gmail.com*	Profesa Emirita, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Profesa Msambichaka ana shahada ya uzamivu (PhD) katika uchumi wa kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Leipzig, Ujerumani. Ni mtafiti na mshauri mtaalam katika eneo la uchumi na maendeleo kwa ujumla kwa miaka mingi.
2. Prof. Joseph J. Semboja *Anwani: S.L.P. 105753, DSM* *Simu: 022 2602916* *Email: pjsemboja@gmail.com*	Prosesa Mshiriki wa Uchumi, UDSM. Aliwahi kuwa mkurugenzi mtendaji wa REPOA na Uongozi Institute. Profesa Semboja ana PhD katika uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Illonois, Marekani. Eneo lake la ubobezi ni fedha za umma na maendeleo ya kitaasisi.
3. Balozi Dkt. Asha Rose Migiro	Balozi mstaafu wa Tanzania nchini Uingereza. Aliwahi kuwa Naibu

Jina na Taarifa za Mjumbe	*Muhtsari wa Wasifu wa Mjumbe*
	Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na mhadhiri mwandamizi katika sheria, UDSM. Ana shahada ya uzamivu katika sheria kutoka Chuo Kikuu cha Konstanz, Ujerumani.
4. *Dkt. Florence M. Turuka*	Kwa sasa Dkt. Turuka ni mhadhiri mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Huko nyuma alishakuwa katibu mkuu wa wizara kadhaa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ana shahada ya PhD katika uchumi wa kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Justus-Liebig Giessen, Ujerumani.
5. *Dkt. Amina Suleman Msengwa* *Anwani: S.L.P. 35047, DSM* *Simu: 0784 788266* *Email: msengwa@gmail.com*	Dkt. Amina Suleman Msengwa ni mhadhiri mwandamizi katika takwimu kutoka UDSM. Ana shahada ya PhD kutoka UDSM.
6. *Dkt. Yahya Hamad Sheikh* *Simu: 0777 438903* *Email: yahya.sheikh@suza.ac.tz*	Dkt. Yahya Hamad Sheikh ni mhadhiri mwandamizi katika mifumo ya TEHAMA (informatics) katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (State University of Zanzibar-SUZA) Ana shahada ya PhD kutoka Chuo Kikuu cha Oslo, Norway. Ni mtaalam wa mifumo ya teknolojia ya habari
7. *Dr Maryam Vuai (F)* *Simu: 0778 703867/0676 899889* *Email: Maryam.a.vuai@gmail.com*	Akiwa anafanya kama mchumi katika Taasisi ya Zanzibar Research for Socio-Economic and Policy Analysis (ZRCP), Dkt. Maryam and shahada ya PhD katika maendeleo ya uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Howard, USA.
8. *Bw. Abdul Rajabu Mhinte (M)*	Bw. Abdul Rajabu Mhinte ni Naibu Mkurugenzi wa Uchumi, Ofisi ya Rais. Ana shahada ya pili ya uchumi kilimo (MSc Agricultural Economics) na shahada ya kwanza katika maendeleo vijijini (BSc in rural economy) kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.
9. *Bi. Emmy Kalomba Hudson* *Anwani: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mji wa Serikali, Mtumba,S.L.P. 630, Dodoma* *Simu: 0754 637726* *Email:* *emmyhudson@yahoo.com;* *emmy.hudson2@agctz.go.tz*	Bi Emmy Hudson ni mwanasheria mwandamizi (Principal State Attorney) katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ana shahada ya kwanza (LLB) katika sheria kutoka UDSM and Diploma ya juu katika sheria ya wanawake (postgraduate diploma in women's law) kutoka Chuo Kikuu cha Zimbabwe.
10. *Dkt. Ntuli Angyelile Kapologwe* *S.L.P. 749, Dodoma* *Simu: 0757 499679* *Email:* *nkapologwe2002@gmail.com*	Dkt. Ntuli Kapologwe Mkurugenzi wa Huduma za Kinga, Wizara ya Afya. Ana shahada ya PhD katika afya ya jamii (public health) kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM). Aidha, ni mhadhiri wa kuitwa (adjunct lecturer) katika taasisi kadhaa za elimu na tafiti nchini, ikiwemo NIMR, UDOM.
11. *Bw. Aidan Frederick Eyakuze* *Anwani: S.L.P. 20742, DSM* *Email: aidaneyakuze@gmail.com*	Kwa sasa Aidan Eyakuze ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirila la Twaweza. Ana shahada ya pili katika uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Simon Fraser, Canada na shahada ya kwanza katika uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Trent, Canada. Pia ni mshiriki wa tuzo (fellow) wa Archibishop Desmond Tutu Leadership na mjumbe wa Bodi ya Uongozi ya Afrika (African Leadership Institute).
12. *Bw. Godfrey Kirenga (M)*	Bw. Kirenga ni Mkurugenzi Mtendaji wa SAGCOT Centre Ltd. since 2013. Ana shahada ya pili ya sayansi (entomology) kutoka Chuo Kikuu cha London (Imperial College). Aliwahi kuwa mkurugenzi wa maendeleo ya mazao katika Wizara ya Kilimo.
13. *Eng. Ally Bondo Samaje* *Anwani: Wizara ya Madini, S.L.P. 422, Dodoma* *Simu: 0716 803258*	Eng Samaje ana shahada ya sayansi katika uchumi wa madini kutoka Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Curtin, Australi. Kwa sasa ni Kamishina Msaidizi katika Wizara ya Madini.

Jina na Taarifa za Mjumbe	*Muhtsari wa Wasifu wa Mjumbe*
Email: samaje.ally@madini.go.tz	
14. Dkt. Richard Joseph Kimwaga *Anwani: Ndaki ya Uhandisi, UDSM, S.L.P. 35131, DSM.* *Simu: 0754 265636* *Email: rkimwaga2007@yahoo.com*	Dkt. Kimwaga ni mhadhiri mwandamizi katika uhandisi wa raslimali za maji (water resources engineering), UDSM. Ana shahada ya uzamivu katika uhandisi mazingira kutoka UDSM.
15. Dkt. Richard Shukia (April 1973, M) *Anwani: S.L.P. 35048 DSM* *Simu: 0717 907288* *Email: richardshukia@gmail.com*	Dkt. Richard Shukia ni mhadhiri mwandamizi katika elimu kutoka UDSM akiwa ni mbobezi katika eneo la elimu ya awali (early childhood education). Dkt. Shukia ana shahada ya uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha Linnaeus, Sweden.
16. Dkt. Gladness Ladislaus Salema *Simu: 0713 243661* *gladness.chitama@gmail.com*	Dkt. Gladness Ladislaus Salem ani mhadhiri mwandamizi katika Idara ya Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ana shahada ya PhD kutoka Chuo Kikuu cha Molde, Norway.
17. Bw. Imani Richard Nkuwi *Anwani: S.L.P. 1351, Dodoma* *Simu: 0784 999191* *Email: Imani.nkuwi@maliasili.go.tz and nkuwiimani@gmail.com*	Bw. Imani Richard Nkuwi ni Naibu Kamishina wa Uhifadhi akuhusika na utafiti na mafunzo katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Ana shahada ya uzamili katika sayansi menejimenti endelevu ya mazingira (MSc. in integrated environment management) kutoka UDSM na shahada ya kwanza ya sayansi katika menejimenti ya wanyamapori (BSc. in wildlife management) kutoka SUA.
18. Bi Amne Sued Kagasheki *Simu: 0686 992163* *Email: amnesuedi@shikanagroup.com*	Bi Amne and shahada ya pili katika sheria (LLM) kutoka Chuo Kikuu cha London na shahada nyingine ya pili katika sheria za fedha (LLM in Finance Law) kutoka Chuo Kikuu cha Geneva. Ni mtaalam wa sheria za kimataifa katika biashara na uwekezaji.Kwa sasa ni mkurugenzi wa shirika la Shikana ambalo linajihusisha na kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala ya kisheria ya biashara na uwekezaji katika sekta za kilimo, mafuta, gesi, ardhi, na utalii.
19. Bw. Zahoro Muhaji *Simu: 0786 410406* *Email: zahoromuhaji@gmail.com*	Bw. Zahoro ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Startup Association (TSA). Ni mjumbe wa Bodi za mashirika kadhaa, ikiwemo kwa mjumbe wa Baraza la Uongozi la Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Taasisi ya Sekta Binafsi (Tanzania Private Sector Foundation-TPSF).
20. Dkt. Neema Mduma *Simu: 0713 702661* *Email: neema.mduma@nm-aist.ac.tz*	Dkt. Neema Mduma ni mhadhiri katika uhandisi wa teknolojia ya Habari na mawasiliano (information and communication sciences and engineering) katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arisha (Nelson Mandela African Institute of Science and Technology- NM-A-IST). Ana shahada ya uzamivu katika eneo kutoka NM-A-IST.
21. Bi. Dorice Mgetta (20.7.1994, F) *Anwani: S.L.P. 1671, DSM.* *Email: dmgetta@gmail.com*	Bi Dorice ni mjumbe wa Bodi ya, TanTrade. Ana shahada ya sheria kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe.
22. Bw. Lawrence N. Mafuru (M)	Katibu Mtendaji wa Tume (Katibu wa Timu).

11. ***Mheshimiwa Rais,*** kama ulivyoelekeza, tutausimamia mchakato wa Dira kwa ukaribu katika kuhakikisha kuwa mchakato huu unakuwa jumuishi na shirikishi kwa makundi

yote ya watanzania na kona zote za nchi, kuanzia Pemba hadi Kagera. Matarijio yetu ni kwamba kupitia mchakato huu tutajenga mwafaka wa kitaifa kuhusu malengo yetu kitaifa na kule tunapotaka kwenda katika miaka ijayo. Tunatamani kama ni kutofautiana tutofautiana katika mikakati, mbinu na njia za kufikia maelgno hayo lakini safari yetu iwe moja.

12. ***Mheshimiwa Rais,*** Aidha, pamekuwa na maoni kwamba pengine muda wa miaka 25 ni mdogo katika dira ya maendeleo yenye kuiangalia nchi miaka mingi ijayo na kizazi kijacho. Hivyo, kama ulivyoelekeza, Timu ya wataalam itakusanya maoni pia kuona Dira yetu ijayo iwe na ukomo wa miaka mingapi.
13. ***Mheshimiwa Rais,*** ninaomba nihitimishe maelezo yangu kwa kuishukuru sana Kamati ya Maandalizi kwa kazi nzuri na kubwa waliyoifanya katika kuandaa hafla hii. Kwa kipekee ninamshukuru Ndugu Jungu mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, na Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, na Ndugu Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, kwa uratibu mzuri wa maandalizi.
14. ***Mheshimiwa Rais,*** ninakushukuru tena kwa heshima uliyotupa ya kujumuika nasi katika hafla hii. Ninaomba kuwasilisha.

Mungu Ibariki Tanzania; Mungu Ibariki Afrika.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.